JINA____________________________________________NAMBARI YAKO_____________

SHAHIHI YA MTAHINIWA_________________

TAREHE ________________________________

102/3

KISWAHILI

KARATASI 3

FASIHI YA KISWAHILI

MUDA:SAA 2½

.

.

MAAGIZO

(a) Jibu maswali manne pekee.

(b) Swali la kwanza ni la lazima.

(c) Maswali mengine matatu yatolewe katika sehemu NNE zilizobaki yaani Tamthilia,Riwaya,Hadithi fupi na Fasihi simulizi.

(d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.

(e) Kila swali lina alama ishirini. (20)

1 SEHEMU YA A: SHAIRI (ALAMA 20)

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Kimya changu kimezidi,navunja yangu subira,
Merejeya kwa miradi,kuhitimisha dhamira,
Kukejeli sina budi,niwafunze utu bora,
Nani aali zaidi,wakenya au vinara?

Sirikali bila hadi, ndo kiini cha madhara
Yanopiga kama radi,isokuwa na ishara,
Yamini kuwa gaidi, wakitupora mishahara,
Nani aali zaidi, Wakenya au Vinara?

Wamejifanya hasidi, wasopatana kifikira,
Wana yao maksuudi, kujizombea ujira,
Wakilenga kufaidi,tumbo zao za kichura,
Nani aali zaidi, Wakenya au Vinara?

Nchi yetu kufisidi, ni jambo linonikera,
Tangia siku za jadi, ufukara ndo king'ora,
Kutujazeni ahadi, nyie mkitia fora,
Nani aali zaidi, Wakenya au Vinara?

Maskini watozwa kodi, wapwani na walo bara

Kwa uvumba na uudi, mwa walipa kwa hasara,

Hamudhamini miradi, mejihisi masogora,

Nani aali zaidi, Wakenya au Vinara?

Mesema kazi ni chudi, basi sirikali gura,

,Nafsi zenu mzirudi,mkubali kuchakura,

Makondeni mkirudi,muondoe ufukara,

Nani aali zaidi,Wakenya au Vinara?

Ujanjenu umezidi, demokrasia bakora,

Debeni takaporudi, michirizi kwenye sura,

Kuwachuja al muradi, kwa za mkizi hasira

Nani aali zaidi,Wakenya au Vinara?

Maswali

(a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (ala 1)

(b) Ainisha shairi hili kwa jinsi tatu na kutoa sababu. (ala 3)

(c) Onyesha mbinu za tamathali lugha katika shairi hili.
(ala 2)

(d) Bainisha matumizi matatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (ala 3)

(e) Andika ubeti wa nne katika mtindo tutumbi. (ala 4)

(f) Fafanua maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili (ala 3)

(g) Taja mpango mmoja unaotajwa kama njia ya kutatua matatizo ya nchi. (ala 1)

(h) Eleza muundo wa shairi hili. (ala 3)

SEHEMU B: RIWAYA.

KIDAGAA KIMEMWOZEA

KEN WALIBORA

Jibu swali la 2 au la 3

2 Lo! Kumbe sumaku ya kaburi yaniotea ili kuanza kunivuta vuu kama kijembe!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala 4)

b) Taja mbinu tatu za lugha kwenye dondoo na utoe mifano (ala 6)

(c) Eleza maudhui yoyote matatu yanayoashiriwa na dondoo hili (ala 6)

(d) Eleza mifano ya wahusika wengine wawili waliovutwa na sumaku ya kaburi. (ala 4)

3. Maudhui ya kutowajibika kwa viongozi imejitokeza wazi katika riwaya ya kidagaa kimemwozea. Thibitisha kauli hii kwa kutoa mifano kumi. (ala 20)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA

MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE

Jibu swali la 4 au la 5

4 "Uvundo haswa! Hata hao wageni sijui wataonaje hali hii. Aibu kubwa inatungoja kama watakuja.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)

(b) Fafanua sifa nne za msemaji wa maneno haya. (ala 4)

c) Kwa kutolea mifano taja mbinu moja ya utunzi inayojitokeza katika dondoo hili. (ala 2)

(d) Mbali na uvundo unaorejelewa katika dondoo hili,jadili uvundo mwingine unaojitokeza katika baraza la mji wa Cheneo. (ala 10)

5. Mwandishi wa mstahiki meya amepata ufanisi mkubwa katika matumizi ya jazanda. Fafanua kwa kutolea mifano katika tamthilia. (ala 20)

SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE – KEN WALIBORA NA S.A. MOHAMED.

Jibu swali la 6 au la 7.

6 "Wee hu kiwetu,babu ee! Neno kwa neno, ngumi kwa ngumi"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala 4)

(b) Mzungumzaji alipewa ushauri tofauti na watu wengine. Eleza ushauri huu na ya mzungumziwa kuhusu ushauri huo. (ala16)

7. Jadili ufaafu wa anwani za hadithi zifuatazo (ala 20)

(i) Mke wangu

(ii) Shaka ya mambo

(iii) Gilasi ya mwisho makaburini

(iv) Kanda la usufi.

SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

8. Eleza maana na umuhimu wa hadithi zifuatazo katika jamii. (ala 20)

(i) Visasili

(ii) Hurafa

(iii) Hekaya

(iv) Mighani